IELEWE SIRI YA

# MSAADA WA BWANA

## KWENYE MAISHA YA MTU



JAMES KALEKWA

# SIRI YA MSAADA WA BWANA KWENYE MAISHA YA MTU

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

**Tabaruku**.......................................................................... 4

**Salamu na Utangulizi**........................................................ 5

Sura ya Kwanza:............................................................ 7

*Uweza wa Mungu dhidi ya Ukomo wa Mwanadamu*...........7

SURA YA PILI:............................................................... 21

*Upekee wa Kiwango cha Msaada wa Bwana*.................... 21

Sura ya Tatu:.................................................................. 27

*Chaguo ni moja na la Pekee*............................................ 27

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarif aya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwoana anvyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mnwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.
3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema. Na heri ya kuzaliwa kwa Pastor JK.

Frida James Kalekwa
Mke wa mwandishi

Juni, 2023
Dodoma, Tanzania

## Sura ya Kwanza:

*Uweza wa Mungu dhidi ya Ukomo wa Mwanadamu*

Kwenye sura hii, nimekusudia kufanya ulinganifu baina ya Mungu na mwanadamu ili kukuonyesha uhitaji wako wa msaada wa Mungu. Sasa kabla hatujaenda umbali huo, basi tutazame mambo ya kimsingi kuhusu msaada wa Bwan kutoka kwenye maandiko matakatifu.

> *Maana Wewe umekuwa msaada wangu, Na uvulini mwa mbawa zako nitashangilia.*
> **(Zab 63:7 SUV)**

Mwanadamu yeyote ana ukomo - hapa ninamaanisha wewe na yeyote unayemtegemea kukusaidia. Kuna mipaka ya kiungu na ya ulimwengu wa roho ambayo mwanadamu hawezi kuivuka. Kuna umbali ambao mwanadamu hawezi kwenda. Hayo yote ni kuonyesha na kumkumbusha tu mwanadamu ya

kwamba yeye ni mwanadamu. Vilevile kuna madhaifu na mapungufu ambayo mwanadamu anayo... mengine yako kimaumbile, kiufahamu, kiuzoefu, kijiografia, kihistoria n.k ambayo mengine anayafahamu na mengine hayafahamu. Kuna mengine yuko kwenye majaribio ya kuyapunguza na kuna yale yaliyo juu ya uwezo wake.

Na kuna aina ya ukomo ambao uko kwa mwanadamu ambao hata yeye mwenyewe haufahamu. Ni eneo ambalo mwanadamu ni kipofu kuhusiana na yeye mwenyewe.

Yote hayo ni kuonyesha hitaji halali na la lazima la mwanadamu kwa msaada wa Bwana. La sivyo atabaki kuwa kama wanadamu wengine kama maandiko yasemavyo...

> "**Hawajui wala hawafahamu, hutembea gizani;** Misingi yote ya nchi imetikisika. Mimi nimesema, Ndinyi miungu, Na wana wa Aliye juu, nyote pia. **Lakini mtakufa kama wanadamu,** Mtaanguka kama mmoja wa wakuu."
>
> Zab 82:5-7 SUV

Kutojua hufungulia hali ya kuenenda kwenye maisha kwa namna ya ukawaida ambayo hupelekea kuwa na mwisho wa kawaida sana. Mwisho kama wanadamu wengine.

Ni vyema ukajua mpendwa wangu ya kwamba BWANA asipohusika katika kumsaidia mwanadamu kwenye nyanja yoyote ya kimaisha; bidii zote za kibinadamu hupoteza maana na huwa hazizalishi matokeo yaliyokusudiwa.

> *"BWANA asipoijenga nyumba Waijengao wafanya kazi bure. BWANA asipoulinda mji Yeye aulindaye akesha bure. Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, Na kukawia kwenda kulala, Na kula chakula cha taabu; Yeye humpa mpenzi wake usingizi."*
> Zab 127:1-2 SUV

Hakuna siku nilisikia kama kutenguliwa nguvu na hali ya kujitumainia kama siku andiko hilo juu lilipofunuliwa

na Roho Mtakatifu na kuwa dhahiri kwangu. Nilijifunza kuheshimu na kuongeza bidii kwenye chochote ninachokifanya... hata hivyo, nikajua kwa yakini kwamba mimi ni tegemezi sana kwenye msaada wa BWANA. Pale ninapodhania niko kwenye kiwango cha juu sana cha utendaji wangu, kumbe niko sakafuni au chini ya sakafu ukiniondolea msaada wa Bwana. Kila mara huwa ninaimba moyoni mwangu,

*"Yesu nakuhitaji, vivyo kila saa*
*Niwezeshe mwokozi, nakujia."*

Kwenye lugha ya kiingereza inasikika kwa uzito zaidi...

*"I need You, oooh I need You*
*Every hour I need You*
*Ooh Bless me now my Saviour*
*I come to You."*

Hebu tusogee mbele zaidi ili uone hitaji la msaada wa Bwana kutokea kwenye ukomo wa mwanadamu.

*26. Ikawa mfalme wa Israeli alipokuwa akipita ukutani, mwanamke mmoja akamwita akisema, Unisaidie, bwana wangu, mfalme. 27. Akasema,* ***BWANA asipokusaidia, nikusaidieje mimi?*** *Ya sakafuni, au ya shinikizoni?*

**(2 Fal 6:26-27 SUV)**

Utaelewa ni kwa nini neno linasema... emalaaniwa amtumainiaye mwanadamu.

*5. BWANA asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha BWANA. 6. Maana atakuwa kama fukara nyikani, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani palipo ukame, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu.*

**(Yer 17:5-6 SUV)**

Kumtegemea mwanadamu ni kutegemea nguvu kutoka kwenye chanzo chenye upungufu wa nguvu - ni kujitafutia laana. Laana ni nguvu inayokuwezesha kushindwa! Mtu aliyelaaniwa hajitahidi kushindwa... unajikuta unaweza tu kushindwa.

Ukomo wa mwanadamu na uweza wa Mungu:

1. Mungu anajua mambo yote kwa wakati mmoja (omniscient) wakati mwanadamu hawezi kujua mambo yote kwa wakati mmoja. Mungu anajua mambo yote yaliyopita, yaliyopo na yajayo; anajua mambo yote yanayoonekana na yasiyoonekana (ulimwengu wa mwili na ulimwengu wa roho).

Iwapo mwanadamu hatasoma historia au kusimuliwa kuhusu mambo yaliyopita au mambo ya kale, basi kuna mambo yatakuwa kama vile hayajawahi kuwepo (non existing) kwake. Iwapo mwanadamu asipoambiwa na kufunuliwa yanayoendelea kwenye ulimwengu wa roho (wengine huuita ulimwengu wa yasiyoonekana), basi kuna kweli ambazo atadhani hazipo. Iwapo mwanadamu hatasaidia kujua kuhusu mambo yajayo, basi kwake hayo yatakuwa si kweli.

Hebu waza kwa namna ya kawaida tu ya kisayansi, kuna baadhi ya vijidudu huwa havionekani kwa macho ya nyama mpaka kutumia hadubini (darubini ya vidudu). Bila msaada wa kifaa hicho, hivyo vijidudu kwake vitakuwa havipo. Ile ya kwamba yeye havioni haiwezi kumaanisha ya kwamba ni kweli havipo. Atadhurika na

hatapata msaada wa aina yoyote wa kimatibabu kwa kuwa hana "msaada wa hadubini". Mapungufu ya wanadamu, yanaonyesha uhitaji wa msaada.

2. Mungu yuko kila mahali kwa wakati mmoja (omnipresent). Wakati huu ninapoandika kitabu hiki hapa Dodoma - Mungu yupo! Wakati wewe unasoma kitabu hiki, popote ulipo sasa - Mungu yupo! Mungu yupo ndani ya muda na nje ya muda.

> "*Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko. Kama nikisema, Hakika giza litanifunika, Na nuru inizungukayo ingekuwa usiku; Giza nalo halikufichi kitu, Bali usiku huangaza kama mchana; Giza na mwanga kwako ni sawasawa.*"
>
> Zab 139:7-8, 11-12 SUV

Mpendwa wangu, wewe huwezi kuwa sehemu nyingi kwa wakati mmoja. Siwezi kuwa Dodoma na Bangladesh kwa wakati mmoja; Siwezi kuwa nyumbani

kwangu na kanisani kwa wakati mmoja; huwezi kuwa darasani na shambani kwa wakati mmoja. Giza lina uwezo wa kukuzuilia usione baadhi ya yanayoendelea huko.

Kwa mfano, mimi ni baba mzazi wa watoto wanne mpaka sasa. Hata nijitahidi vipi, siwezi kuwa kwenye madarasa ya watoto wangu kila mara wakati huo huo niwe ofisini kwangu, kanisani. Kwa hiyo, kama ninataka kujua kuhusu hali ya watoto wangu walio mbali nami wakati huu... basi ninapaswa kutegemea kwenye msaada wa Mungu. Jicho langu haliwezi kuwatazama muda wote; mkono wangu hauwezi kuwafikia masaa yote.

Siwezi kuina kila mshirika ninayemchunga akiwa kwenye mradi wake, ofisini, shambani, darasani, nyumbani, safarini... kama mchungaji ninayewapenda sana watu ninaowalea, ningependa iwe hivyo. Lakini mimi si Mungu. Hiyo ni kuonyesha ya kwamba ninauhitaji sana msaada wa Bwana wa muda wote.

Watu wengi sana wamejizawadia matatizo ya afya ya moyo na akili kwa kujaribu kuwa kila mahali... kuwalinda wenzi wao; kufuatilia maisha

ya kila mtu na taarifa zake za kina (details) anayehusiana nao. Rafiki, kama una mwenzi (mke au mume) au una mchumba ieleweke wazi ya kwamba kamwe hutoweza kuwa mahali alipo muda wote. Unahitaji msaada wa Bwana.

Hata shetani ambaye ni kiumbe roho, hawezi kuwa kila mahali kwa wakati mmoja.
Hata malaika wenyewe, hawawezi kuwa kila mahali kwa wakati mmoja.
Bila msaada wa Mungu hakuna namna utatatua upungufu huu wa kibinadamu.

3. Mungu ana uweza wote (omnipotent) - Mungu anao uweza wote.
Hakuna kitu ambacho unaweza ukakifikiri ambacho kiko juu ya uwezo wa utendaji wa mkono wa Mungu. Kati ya kweli zitaupa moyo wako kupumzika, ni kujua ya kwamba Mungu anaweza mambo yote... nikifundisha dhana za namna hii kanisani, huwa ninauliza swali kama hili "Yote maana yake ni mangapi?" Jibu utakalolisikia

ni hili "Yote". Mpendwa wangu, yote maana yake ni yote. Hata utafute kwa kiebrania kisha kiyunani na lugha yoyote uijuayo. Hitimisho litakuwa yote ni yote! Na hayo ndiyo Mungu awezayo kuyafanya.

Hebu tutazame maandiko ili kujenga uelewa wetu kwenye neno na si fikra za kibinadamu:

> "Aa! Bwana MUNGU, tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyoshwa; hapana neno lililo gumu usiloliweza;”
> Yer 32:17 SUV

> "kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu."
> Lk 1:37 SUV

> "Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda BWANA? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume." Mwa 18:14 SUV

"wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, Tunaye

baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."
Mt 3:9 SUV

"Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana." Mt 19:26 SUV

"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika."
Ayu 42:2 SUV

"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;"
Efe 3:20 SUV

Kwa ushahidi huo mwingi wa kimaandiko nilioutanguliza hapo juu sina namna nyingine ya kukusaidia isipokuwa kukualika uimbe nami utunzi huu...

*"... kwani ni jambo, lipi hilo, Yeye asiloliweza*

*Liseme, Liseme*

*Litaje, litaje*

*Kwani ni jambo, lipi hilo, Yeye asiloliweza..."*

Udhaifu wako kama mwanadamu ni kwamba huwezi mambo yote. Na huo ndiyo unakupa kujua ya kwamba unauhitaji msaada wa Bwana kwa namna ipitayo kawaida.

Hebu fikiria unasaidiwa na anayeweza mambo yote!

Hebu jenga taswira wanadamu wanapoishia, Yule anayekusaidia ndiyo huanzia hapo kwenda kusikofikirika!

## SURA YA PILI:

*Upekee wa Kiwango cha Msaada wa Bwana*

Kwenye sura hii nimekusudia kukuonyesha upekee na umaalum wa msaada wa Bwana. Ningependa uone ya kwamba msaada wa Bwana si mmojawapo bali ni wa pekee! Haupo kwenye machaguo yaliyopo. Msaada wa Bwana "unacheza kwenye ligi yake wenyewe"!

Mwanadamu na mifumo itakupa msaada lakini hautafikia kiwango cha msaada Mungu.

Jambo hili nilifundishwa na Roho Mtakatifu nikiwa kijana mdogo (teenager) ya kwamba kuna mahitaji ambayo watu wangu wanaonipenda na kunitakia mema hata wangetaka kunisaidia lakini hawataweza. Wakati mwingine wanaishia kuumia moyo, kusononeka

na hata kujilaumu. Kuna msaada hawawezi kuutoa kwa kuwa wao ni wanadamu na wana ukomo wao!

Kuna kiwango cha mahitaji yako hakuna mzazi, mwenzi, rafiki anayeweza kukikidhi. Jifunze kutambua hilo na kuanza kuchagua vyema kwa kutowalemea wengine lakini pia kwa kujitendea haki kuchagua kwa ubora zaidi, yaani, kuuchagua msaada wa Bwana.

Hebu tusome maandiko kuielewa dhana hii muhimu sana.

*1. Ole wao watelemkao kwenda Misri wapate msaada, na kutegemea farasi; watumainio magari kwa kuwa ni mengi, na wapanda farasi kwa kuwa ni hodari sana; lakini hawamwangalii Mtakatifu wa Israeli, wala hawamtafuti BWANA!*

*2. Lakini yeye naye ana akili, naye ataleta uovu, wala hatayatangua maneno yake; bali ataondoka juu ya nyumba yao watendao mabaya, na juu ya msaada wa hao watendao maovu.*

*3. **Basi Wamisri ni wanadamu wala si Mungu, na farasi zao ni nyama wala si roho;** na BWANA atakaponyosha mkono wake, yeye asaidiaye atajikwaa, na yeye asaidiwaye ataanguka, nao wote pamoja watakoma.*

**(Isa 31:1-3 SUV)**

*Ni kweli, msaada haufai unaotazamiwa kutoka milimani, makutano yenye mshindo juu ya milima;* ***ni kweli, wokovu wa Israeli ni katika BWANA, Mungu wetu.***

**(Yer 3:23 SUV)**

Iko mifumo imewekwa ili kuyapangilia na kuyasaidia maisha ya mwanadamu awapo hapa duniani.

Ipo mifumo ya serikali za wanadamu.
Ipo mifumo ya sheria na haki.
Ipo mifumo ya uchumi na fedha.
Ipo mifumo ya mawasiliano.
Ipo mifumo yanusafirishaji na uchukuzi.
Ipo mifumo ya elimu.
Ipo mifumo ya afya.

Halafu hiyo mifumo inaongozwa na wanadamu. Kumbuka tumesema wanadamu wana ukomo na udhaifu.

Kwa misingi hiyo basi, hata mifumo iliyopo ya wanadamu imejaa mianya (loopholes) ambayo hupitisha udhaifu wa mwanadamu. Hata mifumo yetu ya hapa duniani. Iwe yabtaifa lolote lile. Hata mifumo inayosifiwa kuwa ni bora kama vile mfumo wa siasa na utawala uitwao DEMOKRASIA. Hiyo nayo ni dhaifu kwa sababu imebuniwa, imewekwa na inaendeshwa na wanadamu kiutekelezaji.

Kwenye maandiko ambayo tumeyasoma hapo juu utaona kuwa kuna mahali palikuwa ni eneo la makimbilio ili kutafuta msaada…. Panaitwa Misri! Ndiyo umesoma vyema. Mahali ambapo njaa kali ilipoikumba dunia ya wakati huo, watu walikimbilia Misri kutafuta msaada wa chakula. Yesu akiwa mtoto mchanga alikimbizwa Misri kama mkakati wa ukoaji wa dharula. Misri ilikuwa na jeshi imara, mifumo ya kiroho (ibada za miungu) thabiti, uimara wa kiuchumi, mfumo wa kisiasa usioweza kutikiswa kwa urahisi.

Hata hivyo, neno limetuonyesha ya kwamba "***Basi Wamisri ni wanadamu wala si Mungu, na farasi zao ni nyama wala si roho;…"***

Hiyo ni kusema kule ambapo mwanadamu anataka kujaribu kuweka tumaini au kuangalia msaada upatikanao huko. Nako ni wanadamu tu! Hawana msaada wa kiwango cha Mungu. Tena kimsingi, wao ndiyo wanaihitaji msaada wa kiungu kutoka kwa Yehova… wamisri siyo Mungu! Wazungu siyo Mungu! Wazazi siyo Mungu! Wazazi siyo Mungu!

Hii ikujengee kujua ya kwamba namna ambayo anaweza kukusaidia Mungu, wamisri hawawezi. Namna anavyoweza kukulinda Mungu, farasi wa vita hawawezi. Namna anavyoweza kukutosheleza nafsini na kukujaza na furaha huyu Mungu wetu, hakuna mwenzi au rafiki anaweza.

Ukiijua hii siri, utawapunguzia watu mizigo… unajua kuna nyakati huwa tunakuwa mizigo kwa watu wengine.Pia, itakusaidia kupunguza kiwango cha matarajio kwa wanadamu ili uwe salama nafsini mwako!

Kuna Amani ipitayo akili zote.

Kuna Amani iliyo juu ya fahamu zote.

Kuna furaha ya Bwana.

Hakuna mume/mke anaweza kutoa; hakuna mzazi; hakuna shule…. Wala hakuna Misri wala farasi wa vita.

## Sura ya Tatu:

*Chaguo ni moja na la Pekee*

Kwenye sura hii nimekusudia kukuonyesha kwa mkazo na kwa kifupi ya kwamba msaada wa Mungu ndiyo msaada pekee na mmoja unaouhitaji. Si swala la kuwa na machaguo (multiple choices). Kwa sababu, huhitaji kuwaza mara mbili juu ya chaguo hili. Ukweli ni huu kuna hali/mazingira huitikia kwenye msaada wa Bwana tu.

*1. Nitayainua macho yangu niitazame milima, Msaada wangu utatoka wapi? 2.* ***Msaada wangu u katika BWANA,*** *Aliyezifanya mbingu na nchi.*
**(Zab 121:1-2 SUV)**

Kutegemea msaada wa BWANA ni kuajiandikisha kwenye kambi ya uheri (kubarikiwa) - Baraka maana yake ni nguvu ya Mungu juu ya mtu kumuwezesha kufanikiwa. Huhitaji kujitahidi, bali unaweza tu

kufanikiwa kwa sababu uwezesho wa kiungu umekukalia tayari. Hebu tazama maandiko hapa chini:

***Heri ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake****, Na tumaini lake ni kwa BWANA, Mungu wake,*

**(Zab 146:5 SUV)**

***U heri, Israeli.*** *Ni nani aliye kama wewe, taifa lililookolewa na BWANA!* ***Ndiye ngao ya msaada wako,*** *Na upanga wa utukufu wako; Na adui zako watajitiisha chini yako, Nawe utapakanyaga mahali pao pa juu.*

**(Kum 33:29 SUV)**

Fahamu ya kwamba kuna hali za kimaisha huja; kuna nyakati hutokea na kuna mazingira huibuka ambayo yanakuwa kama na hali ya usugu fulani. Hayaheshimu jina, nafasi, umiliki wako; hayaitikii kwenye chochote ulichojikusanyia kwenye ghala lako.

Mambo ya namna hiyo hudhibitiwa kwa msaada wa Bwana tu!

Hebu sasa uwe makini kufuatilia maandiko na ufafanuzi wake unaofuata hapa chini ili kujenga imani yako vyema:

a) Msaada wa BWANA utakupa matokeo yasiyo ya kawaida/ya kibinadamu

*Maana kwa msaada wako* ***nafuatia jeshi,*** *Kwa msaada wa Mungu wangu naruka ukuta.*

**(Zab 18:29 SUV/2 Sam 22:30)**

Si kawaida mwanadamu kufukuza jeshi. Hilo jambo hawezi hata kujaribu kufikiri. Mtu yeyote anayesaidiwa na Bwana huwa anafikia hadhi ya kuwa mtu mmoja sawa na jeshi hayo ni matokeo ya msaada wa BWANA.

b) Msaada wa BWANA utakufanya uthibitike (establishment) - unakaa eneo moja bila kutikiswa/kuhamishwa au kusogezwa kando.

*Asiuache mguu wako usogezwe; Asisinzie akulindaye;*

**(Zab 121:3 SUV)**

c) Msaada wa BWANA unakufanya usiwe muhanga wa mazingira na matukio - kuna namna utainuka juu ya hayo.

*"Jua halitakupiga mchana, Wala mwezi wakati wa usiku."*

**(Zab 121:6 SUV)**

d) Msaada wa BWANA unakufanya ushinde kila viunzi na vizuizi mbele yako

*Maana kwa msaada wako nafuatia jeshi, Kwa msaada wa Mungu wangu* ***naruka ukuta.*** **(Zab 18:29 SUV/2 Sam 22:30)**

e) Msaada wa BWANA unakufanya kuwa mtu wa mambo makuu.

*"Kwa msaada wa Mungu tutatenda makuu, Maana Yeye atawakanyaga watesi wetu."* **(Zab 108:13 SUV)**

f) Msaada wa BWANA unakufanya kutenda mambo complex (siyo complicated)

"*Akafanya katika Yerusalemu mitambo ya vita, iliyobuniwa na watu wastadi, iwekwe juu ya minara na juu ya buruji, ili kutupa mishale na mawe makubwa. Jina lake likaenea mbali sana; kwa kuwa alisaidiwa mno ajabu, hata akapata nguvu."*

(2 Nya 26:15 SUV)

g) Msaada wa BWANA unakuepusha na uonevu wa namna yoyote wa maadui.

*Ikawa maakida wa magari walipomwona Yehoshafati, wakasema, Mfalme wa Israeli ni huyu. Basi wakamgeukia ili wapigane naye; lakini Yehoshafati akalia, na BWANA akamsaidia; Mungu akawafarakisha kwake.*

**(2 Nya 18:31 SUV)**

Kwa kuchagua kusoma kitabu hiki… tayari ninakusikia kwenye maombi unauita msaada wa Bwan; Ninakuomba unavyokiri na kutangaza. Ninakuona kwa mayo ya Imani jinsi unavyoruka juu kama tai.

Nimekuombea kwa Bwana ya kwamba kuanzia leo, utakuwa mnufaika wa msaada wa BWANA!

NEW VINE CHURCH | Dodoma



## Kuhusu New Vine Church

New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)*.

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



## Mahali tulipo

Swaswa, mkabala na geti la Waziri Mkuu,
Dodoma mjini

## Ratiba za Ibada

| | |
|---|---|
| **Alhamis** | Saa 11.15 jioni - saa 12.15 jioni |
| **Jumapili** | Saa 3.00 asubuhi - saa 6.30 mchana |

nvc_dodoma
+255 769 240 777

## Kuhusu Mwandishi



Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa "Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari." [Habakuki 2:14]

## Mawasiliano na Mwandishi


wapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

- James Kalekwa
- james_kalekwa
- @MchungajiJK
- James Kalekwa

---

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia **+255-754-917-7764** (Kupiga simu, SMS na WhatsApp).